# MWONGOZO WA MATUMIZI YA FEDHA ZINAZOPELEKWA HALMASHAURI KWA AJILI YA UKARABATI AU UJENZI WA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA NCHINI

Utekelezaji wa mradi wa kukarabati na kujenga Vituo vya kutolea huduma za Afya nchini utatumia utaratibu wa "Force Account" ambao ni kwa mujibu wa Ibara ya 17 ya Kanuni ya Sheria ya manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 ili kupunguza gharama na kuongeza ubora wa majengo yatakayo jengwa. Juhudi mbalimbali za upatikanaji wa rasilimali Fedha kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Wizara ya Afya, Fedha na Mipango na Wadau wa Maendeleo kufuatia mpango mkakati wa maboresho ya huduma za Afya.

Yafuatayo ni maelekezo ambayo yanapaswa kuzingatiwa na Mikoa na Halmashauri zote wakati wa kusimamia utekelezaji huu tangu kuanza utekelezaji mwaka 2017/18.

1. Fedha zitatumwa kwenye akaunti ya Halmashauri au ya kituo cha Afya husika. Maamuzi ya uchaguzi wa akaunti ya kutumia yazingatie urahisi wa kutekelezaji wa wake.

2. Mfumo wa matumizi ya fedha utakaotumika ni wa "Force Account" ambao utatekelezwa na Taasisi Nunuzi kwa kusimamia ujenzi, kutumia wataalamu na vifaa vyake, kuajiri watumishi/vibarua wa muda na au kwa kushirikisha taasisi za Umma. Utekelezaji wake utakuwa kama ifuatavyo;

   (i) Kubainisha mahitaji yote kabla ya kuanza kazi kwa kuwahusisha wataalamu wanaohusika.

   (ii) Kubainisha atakayefanya kazi (mjenzi), atakayesimamia, watumishi/vibarua wa muda na gharama zitakazohusika na muda wa utekelezaji hadi kazi kukamilika. Njia zifuatazo zitumike wakati wa manunuzi na kupata mafundi/vibarua wakati wa kutekeleza mradi;

      a. Hati Msako (Quotation)itakayozingatia uzoefu
      b. Ushindani Mdogo (Mini Competion)
      c. Manunuzi ya Moja kwa Moja (Single Source)



Scanned by CamScanner

3. Kuomba kibali cha kufanya kazi kwa kutumia njia ya "Force Account" kutoka Bodi ya Zabuni na Kamati ya Fedha na Uchumi ya Halmashauri husika.

4. Kuunda Kamati mbalimbali kwa ajili ya kusimamia utekelezaji kama ifuatavyo:-

    - Kamati ya Ununuzi – Katibu wake awe ni Afisa Ugavi.
    - Kamati ya Mapokezi – Mhandisi, Mkadiriaji Majenzi (QS) au Mbunifu Majengo (Architect) awe miongoni mwa wajumbe wa Kamati.
    - Kamati ya Ujenzi – Mhandisi na Mchumi wawe miongoni mwa wajumbe wa Kamati
    - Kamati ya kijiji na Kamati ya kusimamia kituo cha Afya zihusishwe kikamilifu ili zisaidie katika usimamizi na uangalizi wa kila siku wa ukarabati/ujenzi wa kituo cha afya.

5. Watakao husika au kuajiriwa wakati wa utekelezaji wa kazi wathibitishwe na Mamlaka husika.

6. Bidhaa zinapaswa kununuliwa kwa bei ya Soko au kiwandani ili kupata thamani ya fedha.

7. Nyaraka mbalimbali kuhusiana na Ujenzi/Ukarabati zihifadhiwe vizuri kwa ajili ya kumbukumbu na rejea za mara kwa mara ikiwemo ukaguzi.

Mgawanyo wa majukumu ya utekelezaji utakuwa kama ulivyoanishwa hapa chini: -

(i) Wahandisi, Mafundi na Wataalamu wengine katika Halmashauri watahakikisha viwango vya ubora vinavyohitajika vinafikiwa kwa kusimamiwa kwa karibu hatua zote za ujenzi.



Scanned by CamScanner

(ii) Mhandisi wa Sekretarieti ya Mkoa atahakikisha ubora wa majengo uliokusudiwa unafikiwa kwa kujenga ufuatiliaji.

(iii) Mkurugenzi awasilishe taarifa za utekelezaji za mradi huu kwa Katibu Tawala wa Mkoa ili aziwasilishe OR – TAMISEMI kila tarehe 05 ya mwezi unaofuata, na Halmashauri zote zenye mradi kuwasilisha kwa Makatibu Tawala ifikapo tarehe 30 ya kila mwezi kuonyesha hatua za utekelezaji.

(iv) Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto zitafanya ufuatiliaji na tathmini (M&E).

(v) Taarifa ya maboresho ya huduma za Afya pia zinahitajika ili kuwezesha kuwa na ufahamu namna huduma zilivyoboreshwa, kwa kuwa na ongezeko la wagonjwa kwenye vituo, kupungua kwa kero zinazotokana na utolewaji wa huduma. Ongezeko la makusanyo ya vyanzo vya ndani, utolewaji wa motisha kwa watumishi ikiwemo on call, n.k.

- Kuongezeka kwa uwajibikaji, weledi, uadilifu na ushirikishwaji.

Usimamizi wa miradi hii ufanyike kwa kuzingatia mpango kazi ili kumaliza kwa wakati na kupata thamani ya fedha iliyokusudiwa.



Scanned by CamScanner